BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Tisa – Tarehe 10 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

57. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Ni lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, kutenga asilimia 10 ya makusanyo yake ya ndani kwa lengo la kuwasaidia vikundi vya wajasiriamali wadogo wadogo kwa kuwapatia mikopo nafuu kupitia vikundi hivyo kwa wanawake, vijana, na watu wenye walemavu ili waweze kujikwamua kiuchumi. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa walengwa juu ya utaratibu huo kutoonekana kiuhalisia.

    (a) Je, kuna taaluma yoyote inayotolewa kwa wadau hawa kujua kuwa ruzuku hizo na wapi zinapatikana.

    (b) Je, katika kipindi cha Januari, 2022 hadi leo hii ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wangapi kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa wamefaidika na mikopo hiyo nafuu.

    (c) Je, ni upi utaratibu mpya wa kupata mikopo hiyo.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

28. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Zipo taarifa za Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) kupoteza kiasi cha shilingi bilioni tisa (9bil.) zitokanazo na jasho la walipa kodi.

    (a) Je, upotevu wa fedha hizo ulisababishwa na kitu gani.

    (b) Je, ni ipi hatma ya kupotea kwa kiwango hicho kikubwa cha fedha.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

27. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kampuni ya MECCO ilishinda zabuni ya ujenzi wa barabara ya Wete - Konde na Wete - Gando. Hata hivyo, ujenzi wa barabara hizo haukuwa wa kiwango cha kuridhisha na Kampuni hiyo imepewa tena kazi ya ujenzi wa barabara kongwe ya Chake - Wete.

(a) Je, ni sababu zipi zilizofanya kampuni hiyo kupewa kazi tena ya ujenzi wa barabara ya njia kongwe.

(b) Je, ni kwa kiwango gani wahandisi wa Wizara yako wameshirikishwa katika kuingia makubaliano na kampuni ya MECCO ya ujenzi wa njia kongwe.

77. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ina nia nzuri ya kuwajengea barabara wananchi wake ili wasipate usumbufu kwa kutumia lami baridi kujenga barabara ambazo tayari zimeshaharibika. Miongoni mwao ni barabara ya Kangani – Mtambile, Mtambile – Kengeja, Ukutini – Chambani na Chanjamjawiri – Tundauwa. Kwa vile barabara hizo hazimo katika orodha ya barabara zitakazojengwa kwa fedha za 'Covid'.

Je, Serikali ina mpango wa kuzijenga barabara hizo ambazo huwezi kuzifikia barabara zilizopangwa kujengwa kwa fedha za 'covid' kama hujapitia au hujazitumia barabara hizo.

Wizara ya Afya:

45. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kuna umuhimu wa wafanyakazi kuwa na vitambulisho ambavyo vitasaidia pia kutambuliwa na watolewa huduma ili kuepusha usumbufu na kurahisisha utoaji huduma.

Je, ni lini Wizara ya Afya itaanzisha utaratibu wa kuwapa vitambulisho wafanyakazi wake ambavyo pia vitaonesha vyeo vyao hususan katika hospitali kubwa ili kuepusha usumbufu na kurahisisha utendaji.

<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>

51. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ni ukweli kwamba Zanzibar hadi sasa tunaitegemea sana Tanzania Bara kupata nishati ya umeme, jambo ambalo limesababisha bei isiyo rafiki kwa taasisi zetu na kwa wananchi wetu walio wengi, Hata hivyo, hali ya kimaumbile ya visiwa vya Zanzibar ni rafiki na inavyo vyanzo mbali mbali na vya uhakika vya nishati ya umeme kama vile Hydroelectric power (HEP), Geothermal electric power (GEP), Solar Electric power (SEP), na Biogas electric power (BEP) ambavyo havijapewa kipaumbele.

(a) Je, ni yepi matokeo ya utafiti wa vyanzo hivi vya nishati ya umeme.

(b) Je, ni lini Serikali itaondokana na nishati tegemezi na kutumia vyanzo mbadala vya nishati ili kuondokana na nishati isiyo ya kudumu wala uhakika.

52. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika Jimbo la Wingwi, viko visima vya maji kadhaa kama vile Meli Tisa, Mapofu, Mvumoni Kilindini, Michungani, Njuguni na Sizini ambapo visima hivyo hadi sasa havina walinzi na kwa hivyo kuhatarisha usalama wa maji yake na miundombinu husika.

(a) Je, Serikali inahakikishaje usalama wa maji kutoka katika visima kama hivyo kwa matumizi ya binaadamu na wanyama.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuajiri walinzi kwa ajili ya vianzio hivi muhimu vya maji.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

65. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika msimu wa uchumaji wa karafuu wa mwaka 2021/2022 na hata msimu uliopita huko nyuma, kuna watu wengi walioanguka mikarafuuni na mpaka sasa bado hawalipwa fidia zao.

(a) Je, Wizara imechukua hatua gani katika kuhakikisha wananchi wanalipwa fidia hizo.

(b) Je, mpaka sasa ni watu wangapi wameshalipwa fidia zao.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

33. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kutambua umuhimu wa historia ya nchi yetu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuiendeleza nyumba ya Makumbusho iliyopo Kijangwani.

(a) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kutekeleza azma hiyo ya Serikali.

(b) Je, kwa wakati huu nyumba ya Kijangwani iko katika hali gani.

(c) Je, kwa nini utekelezaji wa shughuli za makumbusho hayo hazikufanyika katika Bajeti ya Wizara yako kwa mwaka 2021 – 2022.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

46. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kama inavyofahamika kwamba ndani ya visiwa vya Zanzibar tunayo rasilimali muhimu sana ya misitu kama vile msitu wa Jozani kwa Unguja na msitu wa Ngezi ulioko Micheweni, Pemba. Kwa kiasi kikubwa rasilimali hii imekuwa ni moja kati ya vivutio vikubwa vya watalii wetu na wengi wao huitembelea misitu hiyo

kwa shughuli mbali mbali za kitalii ikiwemo Utalii wa Masomo.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichopatikana kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022 kutokana na matumizi ya rasilimali hii ya misitu ya Zanzibar kutoka kwa watalii wa ndani na nje.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kutokana na rasilimali nyengine zilizomo katika misitu ya Zanzibar.

67. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika azma yake ya mwaka wa fedha 2021/2022 programu ya uhifadhi wa maendeleo ya misitu ilipanga kujenga mabanda matatu ya mfano wa kufugia nyuki katika Wilaya ya Micheweni, Kusini na Kati, pamoja na kutoa mafunzo ya ubora wa uzalishaji wa asali isiyokuwa na kemikali (*organic honey*) kwa wakulima mia tatu (300).

(a) Je, Wizara imefikia hatua gani katika utekelezaji.

(b) Je, ni wakulima wangapi wamepatiwa mafunzo hayo ya ufugaji nyuki.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

12. MHESHIMIWA ZAINA ABDALLA SALUM (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kutenga skuli maalum za elimu mjumuisho. Hata hivyo, skuli hizo zimekuwa mbali na maeneo wanayoishi wanafunzi wenye ulemavu kwa kutokuweza baadhi yao kupata haki ya msingi kutokana na ulemavu wao.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuziongeza skuli hizo.

(b) Je, skuli ya Elimu Mjumuisho zitakuwemo katika mpango wa Serikali wa kujenga majengo mapya ya skuli.

48. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ni Ofisi inayofanya kazi zake za ukaguzi na tathmini ya walimu na maendeleo ya wanafunzi. Hata hivyo, Ofisi hiyo inafanya kazi katika mazingira magumu na yasiyoridhisha na zaidi haifanyi kazi kwa uhuru kwani Mkaguzi (Mwalimu aliyeteuliwa) humbidi kumkagua mwajiriwa mwenzake.

(a) Je, ni lini Serikali itaimarisha Ofisi hiyo kwa kuipatia vitendea kazi vya uhakika kama vile usafiri na kadhalika.

(b) Je, ni taasisi ipi ya Serikali inapima ubora na ufanisi wa Ofisi hiyo ya Ukaguzi wa Elimu Zanzibar.

(c) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuiondoa Ofisi hiyo kutoka Wizara ya Elimu na ikabaki kama mamlaka inayojitegemea.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
10 Mei, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA